Umeandikwa na Hope Azeda
Mhariri ni Saumu Mwasimba

## Utangulizi

Hujambo na karibu tena katika kipindi cha sikiliza ujifunze juu ya afya. Natumai bado unakumbuka juu ya maisha ya vijana watano waliotoka kijijini kuja kusoma mjini, Steve, Manuel, Jimmy, Simo na Hassan. Vijana hawa wanaendelea kuishi katika bweni la Mandela ambalo ni sehemu ndogo na chafu ingawa mwenye nyumba wao ana haja tu ya kupokea kodi ya nyumba. Katika kisa cha leo Jimmy bado anaugua maradhi sugu na rafiki zake Manuel, Simo, Hassan na Steve wanajitahidi kumsaidia… Andamana nasi basi ili upate kusikia vipi vijana hawa watakavyoyatatua tatizo hilo. Na mwisho tutakupa maelezo kidogo juu ya chanjo inavyoweza kukusaidia kubakia na afya nzuri.

## Tukio la Kwanza

*Hassan, Jimmy, Manuel na mwenye nyumba kwenye bweni asubuhi. Sauti ya mbu.wavulana wakijiandaa kwenda shule.*

Hassan: Jimmy leo pia huwendi shule?

Jimmy: (Kwa unyonge) Sijisikii vizuri Hassan, nina homa kali na lo, hiki kidonda kinauma kweli.

Manuel: Mimi bado sielewi ulikipataje hicho kidonda.

Jimmy: (Kwa unyonge) Manuel ngoja nikwambie hiki kidonda, kilianza mchezomchezo tu, nilikatwa na bati la mlango wa choo kile, lakini sasa naona kimezidi kimechimbika hasa.

Hassan: Na chatoa kweli, kinanuka ile mbaya, kwa nini hubadilishi bendeji hiyo? Imegeuka rangi na kuwa njano na chafu kabisa!

Manuel: Jimmy nenda ukafungwe kiliniki kabla hakijaingia uchafu! Na kupata maambukizi.

Jimmy: (Kwa unyonge) Manuel nimesikia lecture zako nyingi za afya… sina haja ya kusikia tena nataka kwenda nyumbani mimi kijijini. Kwa sasa nitaendelea tu na kukiosha na chumvi na maji… tosha.

Hassan: Manuel nadhani inabidi tufanye tuwetalo tumsaidie Jimmy aende nyumbani, lakini kwanza lazima tuwatafute Steve na Simo.

Manuel: Ni kweli, pengine wamepata pesa na wakaamua kustarehe, na kusahau kuna mgonjwa ambaye maisha yake yanawategemea wao.

Hassan: Lazima tuondoke sasa kwenda shule, muda umekwisha… Jimmy baadae basi. (Wanaondoka)

Jimmy: (Akoroma kwa maumivu) Ashhhhhhh ayaaayaaa naumwa… naumwa…

Mwenye nyumba: (Anabisha mlango) nimekupata! Enhe nambie ni mchezo gani huu wa paka na panya mnaonichezea, mna njama gani nauliza?

Jimmy: Oh mama, mwenye nyumba… shingo shingo inaniuma (anazungumza kwa maumivu)

Mwenye nyumba: (Kwenye Mic) Una matatizo gani? Acha upuuzi huo na unilipe pesa zangu!

Jimmy: (Akoroma kwa maumivu) Kraaaa aaayiii aohhhhh

Mwenye nyumba: Sasa nakuuliza je Jimmy, unafanya sarakasi au unaumwa kweli? (Jimmy anaanza kutetemeka)

Mwenye nyumba: (Kwa mshutuko) Mungu wangu huyu mtoto atakufa… jamani Mtoto wa watu… Hassan… ah jamani bora nikawatafute hawa kina Hassan na Manuel huko shule… pengine watamsaidia… Mungu wangu mashaka gani haya…

(Jimmy akoroma kwa sauti kubwa kutokana na maumivu makali)

**Tukio la Pili**

*Mwenye nyumba, katibu wa shule, Hassan na Manuel wako kwenye afisi ya usimamizi wa shule, wakati wa mapumziko ya muda mfupi ya wanafunzi. Katibu wa shule akipiga chapa na kushughulika shughulika, sauti za wanafunzi wa kike na kiume zinasikika kwa mbali.*

Mwenye nyumba: Samahani Madam, nahitaji kumuona Manuel na Hassan kwa dharura sana Madam, nimesubiri kwa dakika kumi sasa…

SFX: Acha kupiga typu

Katibu: Subiri nimtume mtu akawaite… hukumuona yule kijana mdogo niliemtuma?

Mwenye nyumba: Ah tangu nilipokuja hapa nakuona ukipipiga hilo dude na vidole… ndo laitwaje hilo mashine? Ah ndio typureta… ah sijui mie… basi huwezi kumtuma mtu haraka akenda kuniitie vijana hao.

SFX Anaanza kupiga chapa tena…

Katibu: Kuwa na subira madam, watakuja sasa hivi usijali!

Mwenye nyumba: Kifo hakisubiri mama!

Katibu: Wataka kufa?

Mwenye nyumba: Sio mimi, rafiki yao! Tafadhali unaweza kuacha kidogo hiyo kazi yako usikilize haya nnayokwambia?

SFX Aacha kupiga taipu

Katibu: Kwa nini… sina muda… nina kazi nyingi sana madam… ok hao vijana wanakuja!

Mwenye nyumba: Njooni haraka sana nyie… sasa hivi twendeni nyumbani!

Hassan: (Anakuja) Manuel usiende! (Anamnong'onezea Manuel sikioni) anatupeleka kituo cha polisi!

Manuel: Niache mkono wangu madam. Kuna nini? Umefuata nini hapa? Turudi zetu darasani Hassan, tunakosa masomo bure!

Mwenye nyumba: Hebu sikizeni nyie… mwenzenu Jimmy ni mgonjwa sana. Mnafikiri naweza kuja huku kote kuwadanganya? Jimmy anahitaji msaada wenu sasa hivi vinginevyo atakufa mwenzenu. (Watu wanong'ona)

Katibu: Hey vijana bora mwende nyumbani mkamtazame mwenzenu.

**Tukio la tatu**

*Jimmy, Manuel, Hassan na mwenye nyumba bwenini.*

*SFX* *Sauti ya mbu*

Jimmy: (Akikoroma kwa maumivu)

Manuel: (Kwa woga) Mungu wangu, Jimmy uko sawa?

Hassan: (Kwa woga) Manuel, lazima tufanye kitu hapa… meno yake yamekamatana sana… hawezi hata kuzungumza… lazima tumsaidie.

Manuel: Tatizo ni kwamba hawezi kusimama wala kutembea Hassan.

Mwenye nyumba: Vijana mnajua hakuna muda wa kupoteza hapa, mwenzenu yuko katika hali mbaya sana… mpelekeni hospitali sasa hivi…

Hassan: Vipi mama mwenye nyumba?

Manuel: Ntachukua baisikeli halafu nikaombe gari la shule.

Hassan: Kama hilo gari litakuwa bado lipo…

Manuel: Ngoja nijaribu Hassan!

Hassan: Nenda basi ukajaribu… jaribu pia kutafuta njia yoyote tupate gari tumsaidie… Jimmy atakufa.

**Tukio la 3**

Daktari, Manuel, Hassan, mwenye nyumba kwenye kliniki.

*SFX* *Hakuna shughuli nyingi; watoto wanalia, wagonjwa wengine wanakohoa na kupiga chafya, sauti mbali mbali zasikika.*

Daktari: Rafiki yenu Jimmy ana dalili za kuugua pepo punda… na maisha yake yako hatarini!

Manuel: Daktari kweli…

Daktari: Tutafanya tuwezalo kumsaidia… unajua bacteria za pepo punda zinasababisha kubana misuli na ikiwa pepo punda inamshika mtu kwenye kinywa basi inasababisha hali ya mdomo kubanwa na kushindwa kufunguka au kufunga.

Hassan: Daktari, sasa basi haugui pepo punda…

Daktari: Nini kinakufanya ufikirie hivyo?

Manuel: Nafikiri Hassan anasema hivyo kwa sababu sio tu kinywa chake kilichokakamaa lakini mwili mzima uko katika hali hiyo…

Daktari: Pepo punda ni maradhi ambayo pia yanaweza kusababisha matatizo ya kubana pumzi, na hii ni hatari sana. Na ukweli wa mambo nawashauri mpate chanjo dhidi ya maradhi haya ya pepo punda sasa hivi.

Manuel: Mama mwenye nyumba wetu ataanza yeye…

Daktari: Basi wakati mnatafakari juu ya hilo, wacha nimtazame Jimmy. (Anaondoka)

*SFX* *Mlango unafunguliwa na kufungwa.*

Mwenye nyumba: Naogopa mimi sindano, nyinyi vijana anzeni nyie! Hassan nenda ukadungwe!

Hassan: Hapana, anza wewe Manuel. Mimi nimesikia kwamba watu wengi wanapata maradhi baada ya kupata chanjo kama hizi.

Manuel: Wacha mchezo Hassan, hizo ni porojo tu za watu tunazozisikia kila wakati.

Hassan: Watu wengine wanasema hizi chanjo za kulazimishwa ni mipango ya serikali.

Manuel: Mimi sijali watu wengine wanafikiria nini kuhusu chanjo za kulazimishwa. Unajua baada ya yote, ni sisi tutakaodhurika ikiwa hatukuchanjwa… hulazimishwi unajua… ni uamuzi wako mshikaji!

Hassan: Ungekuwa uko kanisani unahubiri ningepiga kelele! Hubiri brother! sema wakusikie!

*SFX* *Mlango unafunguliwa na kufungwa*

Manuel: Vipi Dokta Jimmy anaendeleaje?

Daktari: Yuko katika hali nzuri…

Hassan: Sasa anaweza kurudi Ghetto… (akicheka) samahani dokta namaanisha twaweza kwenda nae nyumbani kwetu tunakoishi?

Daktari: Sio kwa sasa. Pengine baada ya siku chache… anahitaji kupumzika kidogo… haya nani ataanza kupata chanjo ya pepo punda?

Manuel: Mi.. mm.. Manuel kwanza.

Daktari: Acha woga kijana… haiumizi…

Hassan: Mimi ntakuwa wa pili baada ya Manuel.

*SFX* *Kiti kinasogezwa, vifaa vya matibabu vinasikika vikigongwa mfuko wa plastiki unafunguliwa.*

Daktari: Ni kidogo tu… nakudunga hapa… halafu kwisha… je umesikia maumivu?

Manuel: Ndo umemaliza daktari? Hata sikuhisi chochote… Hassan wewe je?

Hassan: Sikuhisi maumivu yoyote, lakini hata kama nimehisi maumivu siwezi kukiri sisi ni wavulana wakubwa bwana au sio? Na mabarobaro kama sisi hatulii!

Daktari: Ok vijana kama ni mashujaa namna hiyo kwa nini msije tena mpate chanjo nyingine zaidi?

Manuel: Wakati wetu wa kuondoka umefika, Hassan twende, au tukifanya mchezo baada ya chanjo tutajikuta kwenye meza ya kufanyiwa upasuaji hapa… (wachekacheka)

*SFX* *Sauti za kutembea mwendo wa kasi nje, na mlango unafungwa*

*Muziki*

**Jee unajuwa? Dawa za chanjo**

*Wasemaji wawili, mmoja kwa wale wanaoongoza, na mmoja kwa wengine*

**Ukweli**

Dawa za chanjo zinaweza kuwalinda binadamu na magonjwa mabaya kadhaa na huenda hata magonjwa yanayosababisha vifo. Pale dawa ya chanjo inapotumiwa, inausaidia mwili kujenga kinga. Kinga za mwili ni zile seli za ulinzi. Zinaulinda mfumo wa kinga na kupigana na vitu vilivyo vya kigeni katika mwili, vijidudu, bakteria na virusi.

## Uvumi

Kuna uvumi wa aina mbali mbali barani Afrika kuhusu dawa za chanjo. Baadhi ya watu hutaja hadithi juu ya watu waliokufa au kuwa wandawazimu baada ya kuchanjwa. Wengine hufikiri kwamba dawa za chanjo zimetengenezwa na wataalamu wa nchi za Magharibi ili kuwaangamiza wakaazi wa Afrika. Uvumi huo sio kweli. Ni madaktari wa kweli ndio wanaoruhusiwa kutumia dawa za chanjo kwa wagonjwa, dawa ambazo zimejaribiwa na kupewa kibali kwa matumizi na Shirika la Afya Duniani, WHO. Dawa nyingi za chanjo zina athari chache au hazina athari zozote. Hata hivyo, uvumi sio kwamba hauna msingi wowote, kwa vile kuna madawa bandia ya chanjo ambayo yamesambaa na ambayo ni hatari na yanaweza yakasababisha vifo. Kwa hivyo, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba dawa za chanjo zinatumiwa na madaktari waliosajiliwa katika mahospitali au vituo vy afya. Shauriana na daktari juu ya uwezekano wa kutokea athari za pembeni kutokana na kutumia dawa ya chanjo na vipi ukabiliane na athari hizo.

## Mafanikio

Dawa za chanjo zimetumiwa kwa karne na kila ulipopita muda badhi ya magonjwa yaliokuwa yanasababisha vifo yametokomezwa kabisa. Tunashukuru kwamba kutokana na chanjo, ugonjwa wa nduwi umetokomezwa duniani na kifua kikuu karibu kimetoweka barani Ulaya. Visa vya ugonjwa wa kupooza, Polio, na surua vimepungua sana.

## Mapendekezo

Kuna kampeni duniani za kuendeleza dawa za chanjo kupambana na mafua, surua, kifaduru, dondakoo, pepo punda, homa ya manjano na magonjwa mengi mingine. Shirika la Afya Duniani, WHO, linapendekeza kufanyiwa chanjo za kimsingi kwa watu wote, ikitegemea wapi wanaishi. Vituo vya afya ndio mahala bora kabisa kupata maelezo juu ya chanjo.

## Tamati

Ahsante kwa kujiunga nasi katika kipindi hiki cha Jifunze kwa Kusikia, mlolongo wa wa vipindi vya afya vilivoandikwa na Hope Azeda. Jee unataka kujuwa vipi hadithi hii inavoendelea? Au kuwaambia marafiki zako juu ya hadithi hii? Basi angalia kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/Ibe. Utakuta mlongo wa vipindi vyetu vyote, kukiweko hadithi juu ya ugonjwa wa HIV, wasichana, mazingira na masuala mengi.